Mafanikio

Chama cha HAZINA SACCOS LTD katika utoaji wa Huduma kwa wanachama umepata mafanikio yafuatayo:

1. Katika kipindi cha miaka minne (4) karibuni, chama kimeongeza Idadi ya wanachama kutoka 4504 mwaka 2016 hadi wanachama 5356 katika mwaka wa Hesabu unaoishia Desemba,2018.
2. Chama kimeweza kutoa mikopo mbalimabali kwa wanachama wake.
3. Chama kina ofisi za Huduma katika jingo la Wizara ya Fedha na Uchumi.
4. Chama kimefanikiwa kuajiri wafanyakazi 11 mwaka 2018.
5. Chama kimefanikiwa kukamilisha na Kuwasilisha Hesabu za chama zilizokaguliwa (audited accounts) kwa mujibu wa sheria.

Matarajio

Katika kipindi cha miaka kumi (10) ijayo chama cha HAZINA SACCOS kinatarajia:

- Kupanua uwigo wa wanachama kwa kuwakaribisha wafanyakazi wa sekta na makampuni binafsi na wastaafu.
- Kuanzisha Huduma za Kibenki (FICOS) kwa wanachama wake.
- Kuongeza Idadi ya wanafanyakazi na matawi ya Huduma ili kusogeza Huduma za mikopo kwa wanachama.
- Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi ili kuongeza ufanisi wa kazi na kuweza kukabiliana na mabadiliko ya uchumi, sayansi na teknolojia nchini na ulimwenguni kwa ujumla wake.
- Kutoa Elimu ya Ushirika na Ujasiliamali kwa wanachama ili kuongeza tija kwa shughuli zao.
- Kufungua miradi mbalimabali ya chama kwa ajili ya maendeleo ya chama.

Mahusiano:

Chama kina mahusiano na:

1. **Taasisi za Fedha**
   (a) NBC BANK
2. **Taasisi za ajira za wanachama**:
   (a) Wizara ya Fedha na Uchumi
   (b) Wizara ya Miundombinu
   (c) Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii
   (d) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi
   (e) Wizara ya TAMISEMI
   (f) Wizara ya Kilimo
   (g) Wizara ya Utumishi
   (h) T R A
   (I) P S P F
   (J) Wizara ya Sheria na Katiba
3. **Wadau wa Ushirika nchini**:
   (a) SCCULT

MAKAMPUNI AMBAYO CHAMA KIMEWEKEZA:

1. Kampuni ya Bia Tanzania (TBL)
2. Kampuni ya Sigara Tanzania (TCC)
3. Benki ya CRDB Ltd
4. Kampuni ya Saruji Tanga (Tanga Cement Company)
5. Kampuni ya Saruji Wazo Hill Dar es salaam.
6. Kampuni ya simu ya Vodacom

Kwa mawasiliano na maelezo zaidi, Tafadhali wasiliana nasi kupitia anwani ifuatavyo:

MWENYEKITI,
HAZINA SACCOS LTD,
S L P 9111,
DAR ES SALAAM.

SIMU- +255 (22) 2123026 AU +255 (693) 181 922
+255 (784) 925 953

CHAMA CHA KUWEKA NA KUKOPA CHA HAZINA

(HAZINA SAVINGS AND CREDIT SOCIETY LIMITED)

REG: DRS NO. 1822

HAZINA SACCOS ni nini?

Ni Ushirika wa Akiba na Mikopo kwa ajili ya kuinua, kustawisha na kuboresha hali za wanachama wake.

Historia

Ushirika huu ulianzishwa mwaka 1972 na kusajiliwa rasmi tarehe 21/03/1973 na wanachama wasiopungua 5,356 hadi 2018

Vision:

Ni kuwezesha kukua Ushirika wa Akiba na Mikopo unaotoa huduma za fedha ambazo ni bora, nafuu,rahisi,zinazokidhi na kuridhisha kwa wanachama.

Lengo kuu (General Objective)

Ni kukuza ushirika wenye uwezo wa kujiendesha kwa kulipa gharama zake kukidhi mahitaji ya huduma ya kifedha ya wanachama bila kutegemea asasi/mamlaka/ watu wengine na kutoa msukumo wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii na kuwa sehemu ya mtandao wa huduma za kifedha katika misingi, njia na taratibu za Ushirika.

Malengo Mahsusi (Specific Obejectives):

- Kuweza kukuza na kuendeleza huduma endelevu za kifedha kushiriki na kuhamasisha na kuhimiza uwekezaji wa Akiba, utunzaji salama na uhakika wa Akiba na Hisa.
- Kuweza kujiendelesha kwa faida ili kujiimarisha na hatimaye kujitegemea kifedha na kujitosheleza kiuchumi.
- Kuweza kutoa bidhaa mbalimbali za mikopo zifaazo kwa wanachama.
- Kuweza kutoa Elimu ya **UJASILIAMALI** kwa wanachama.

Huduma zitolewazo:

1. Upokeaji na Utunzaji Akiba na Hisa

(a) **Utunzaji wa Akiba**

Chama hupokea na kutunza Akiba za wanachama ambazo huwawezesha kupata mikopo mara mbili ya kiasi cha mwanachama alichoweka.

(b) Utunzaji wa Hisa

Chama hupokea na kutunza Hisa za wanchama . Hisa hizo huwekezwa na faida hugawanywa kwa wanachama kila mwisho wa mwaka.

2. Utoaji mikopo

(a) Mkopo wa dharura

Kiwango cha juu cha mkopo huu ni 1,000,000na kutoza riba 2% kwa mwezi. Muda wa juu wa marejesho ni miezi 6,hutolewa wakati wowote mwanachama anapokuwa na dharura.

(b) Mkopo wa sikukuuu

Kiwango cha juu cha mkopo huu ni 300,000/ = na kutoa riba ya 1.5%. Muda wa juu wa kurejesha mkopo ni miezi 6 Hutolewa kwa sikukuu za Krismas na Idd Elftri.

(c) Mkopo wa Elimu

Kiwango cha juu cha mkopo huu ni ni 3,000,000/= na kutoza riba ya 1%. Muda wa kurejesha mkopo ni miezi 24. Hutolewa mwezi Januari na Julai.

(d) Mkopo wa maendeleo

Kiwango cha juu wa mkopo huu ni 20,000,000/= na kutoza riba ya 1%. Muda wa kurejesha mkopo huu ni kati ya miezi 12 na 60.Hutolewa mwishoni mwa mwezi na fomu hupokelewa kuanzia tar 1-20 ya kila mwezi.

(e) Mkopo maalumu

Kiwngo cha juu cha mkopo huu ni 30,000,000/= na kutoza riba ya 2%.. Muda wa kurejesha mkopo ni kati ya miezi 12 na 60. Mkopo huu hutolewa pale chama kinapokopa kutoka asasi zingine za fedha.

(f) Mkopo wa Viwanja

Hutegemea na taratibu zitakazowekwa na chama

(g) Mkopo wa Mazishi

Kiwango cha juu ni 3,000,000/= na kutoza riba ya 1% .Muda wa marejesho ni kati ya miezi 12-24 yaani miaka miwili.

(h) Mkopo wa Biashara

Kiwango cha juu ni 20,000,000 na riba ya 1.5% ya baki ya mkopo.Muda ni miezi 12-60**.**

(i) Mkopo wa Ujenzi

Kiwango cha juu ni 30,000,000 na riba ya 1.5%.Muda wa marejesho ni miezi 12-60

MWANACHAMA

Mwanachama wa HAZINA SACCOS LTD ni nani?

Mwanachama wa Hazina SACCOS Ltd ni mtu anayechangia Akiba kila mwezi katika chama hiki.

Je, mtu yeyote anaweza kuwa mwanachama wa HAZINA SACCOS LTD?

HAPANA ila ni mtu yeyote ambaye ni mtumishi wa serikali/Taasisi au shirika la umma.

JINSI YA KUJIUNGA NA HAZINA SACCOS LTD:

- Kujaza fomu ya kujiunga inayopatikana ofisi za HAZINA SACCOS LTD.
- Kulipa Ada ya kiingilio Tsh 20,000/ =
- Kulipa Hisa 10@ Tsh 20,000/=

HUDUMA ZA KIFEDHA

Mwanachama anaruhusiwa kuweka Akiba (savings) au kulipa deni la Hazina SACCOS Ltd kupitia **Benki**.

Malipo yoyote yanyofanyika kwa mwanachama huwa ni kwa njia ya **Hundi**.

Jina la Akaunti—**Hazina Savings and Credit Society Ltd.**

Akaunti namba : **0150237286200**

Benki ya **CRDB**, **Tawi la Holland**.

UKOMO WA UANACHAMA

- Kustaafu kwa kwa mujibu wa sheria
- Kuhamia sekta au makampuni binafsi.
- Kuacha/kufukuzwa kazi serikalini/ taasisi.

KANUNI YA KUTAFUTA RIBA

$$\text{RIBA} = \frac{P\,(N+1)\,r}{200}$$

KIELELEZO:

P– MKOPO
N– MUDA WA KUREJESHA MKOPO
r– RATES (1% AU 2%)